

## The Best Insha KCPE 2008

Andika insha isiyopingua ukurasa mmoja na nusu juu ya kichwa kifuatacho:

MVUA YA GHARIKA KARIANI MWETU

Anza kwa: Wingu kubwa jeusi lilitokea upande wa mashariki. Baadaye matone mazito mazito .....

Yalianza kunyesha. Ngurumo za radi zilihnikiza angani. Watoto walijawa na woga wa shumndwa. Fuadi wangu ulinidwikadwika mithili ya tokomire za wazaramo. MVua

yenyewe itinyesha kwa fujo upepo mkali ulizing'oa paa za nyumba. Tulikaa kimya na kutulia kama maji mtungini tu sijee la kufanya. Chambilecho wamantiki na wananatiki wenye lisani za utaalamu na utalamidhi "Jambo usilolijua ni usiku wa giza.

Baada ya mwia wa kelbu kuukalia mkia, maji yalikuwa yamefurika furifuri na kuingia vyumbani vvyetu. Nilishikwa na huzuni kama mja aliye hukumiwa kunyonga, na sasa yuaongozwa katika kijia chenye giza, na hajui mambo yatakavyokuwa baada ya nukta chache.

Nilikuwa na wazazi wenye fulusi lukuki. Walinifunza na kunienzi kama mboni za maozi yao. Niliishi maisha ya taha mustarehe bimithili ya sultan bin Jerehe. Sasa mali yetu yote yange sombwa na maji. Tulikimbia ili kuyaokoa maisha yetu. Mauti yalikuwa yakitukodolea mdozi. Wengine walibaki nyuma wakisema eti wao ni stadi wa kuogolea. Nasitulikimbia kwani wahenga na wahenguzi wa jaa na jadudi hawakumlazimisha kiwete kuuparanga mti waliponadi. Kwa mwoga huenda kicheko na kwa shujaa huenda kilio.

Katika harakati zetu hizo, tulikutana na asadi wawili. Nilitetemeka bimithili ya kifaranga mwenye manyoya haba wakati wa kipupue. Tulipambana

na hayawani hawa wawili na baadaye  
tukawa shinda. kwani wahenga  
waligunga ndipo waliponadi"  
"Asiyeshindwa si mshindani"

kwa bahati mbaya maji  
yaliongezeka na tuka sombwa sisi  
sote. Hapa kila mtu alitumia ugwiji  
wake ili kuya nusuru maisha yake.  
Nilipiga bismillahi kwa Rabimsta ili  
anipe uwezo wa kuepukana na mauko  
haya. Baada ya muda wa tembe  
kumeza punje la mahindi, nilikuwa  
nchi kavu. Nilimohukuru Rabuka huku  
nikitumai ya kuwa Mungu si mfaki.

"kapu langu lilikuwa tupu na nili hitaji  
maankuli. Ghafila bin vuu nilisikia  
mgurumo wa magari. Loh! Niliona  
magari yaliyo chorwa msalaba mwekundu.  
Nami nilikuwa nimejilaza ardhini  
kwani nilikuwa nimechoka, hoi bin  
tiki tamthili ya punda wa dobi. Niliamka

na kujikakamua hadi magari yalipotia  
habla. Walitoka kwenye gari huku  
wamevaa nguo za kupiga mbizi.  
Walinipea chakula nami nikala kwa  
ulafi kama majuniu wa majunju.  
Manusuta waliokolewa na wengine  
wakapelekwa hospitalini. Tulipewa nguo,  
chakula na mablanketi. Tuliwasifu  
kwa wema wao kwani "chanda  
chema huvikwa Pete

Baadaye, waliopatikwa na mauko walipelekwa kwenye chumba cha kuhifadhi maiti. Mimi mwenyewe niligundua ya kuwa nilikuwa nimefiwa na wavyele wote wawili. Nililia kuikuuikuu. Sikujua nianzie wapi na nimalizie wapi. Mawazo kochokocho yalinizunguka kichwani mwangu.

Wingu la jitimai Lilitanda miongoni mwetu. Baadaye nilipelekwa kwa mbiomba wangu. Ndipo nilipoamini ya kuwa kifo hakina huruma hata chembe.

(alama iliyotuzwa 38)

Insha hii imeandikwa kwa ustadi mkubwa. Kazi imepangwa vizuri kwa sentensi na aya pamoja na hati inayovutia. Makosa ya aina yoyote ni machache sana. Mtahiniwa amejaribu kueleza yaliyotokea akizingatia mada aliyopewa. Hoja zake zimekamilika, na insha yake ameikoleza utamu kwa matumizi ya semi na tamathali. Kosa la tahajia limeonakana:

Mwitu – mwetu

#### 4.3 MAPENDEKEZO KWA WALIMU

- Ni vizuri mfundishe Kiswahili kwa ujumla wake. Tumieni vitabu ambavyo vimependekwa na Wizara ya elimu katika kufundisha.
- Sisitizieni wanafunzi kuwa wakijibu maswali ya kifungu ni lazima wasome kifungu chote ili waweze kujibu maswali, wala wasijikite pale wanapofikiria kuwa swali limetoka.
- Wanafunzi wenu ni lazima wasome kichwa cha insha na kuelewa mada ili waweze kutoa hoja nyingi. Wafundisheni mbinu ya kuzindondoa hoja zao kwanza na kuzikuza katika aya.